

## ***Swahili***

### **Kituo cha Haki za Jumua**

#### **Kituo cha Haki za Jumua ni nini?**

Kituo cha Haki za Jumua (CJC) kimeundwa na Serikali ya Eneo la Kaskazini ili kutoa huduma za upatanisho kwa jumua ili kusaidia watu kusuluhisha mizozo yao bila kuchukua hatua ya kisheria. Huduma yetu ni ya bure, ya siri, kwa hiari, inatolewa kwa wakati wa kufaa na ni rahisi kutumia.

#### **Kwa nini kuchagua upatanisho?**

Upatanisho ina maana watu kuja pamoja ili kujadili maswala ya mzozo. Unawezesha watu wote kwenye mzozo kuwa na la kusema kuhusu matokeo na kufikia wao wenyewe ufumbuzi wa tatizo. Unatoa njia ya kusuluhisha mzozo bila kuchukua hatua ya kisheria ambayo inaweza kuchukua muda na ni ghali.

CJC inatoa mazingira salama na siyo rasmi ambapo watu wanaweza kutatua mizozo yao kwa msaada wa wapatanishi walioelekezwa.

Vikao vya upatanisho kwenye CJC vinatolewa na mpatanishi mmoja au wapatanishi wawili walioelekezwa ambao watakusaidia:

- Kutambua maswala
- Kutafakari njia za kutatua maswala
- Kufikiria hatua nyingine
- Kutumika pamoja ili kufikia maafikiano

Wapatanishi wanatoa muongozo wa jinsi kikao cha upatanisho kinachoendeshwa.

Watu katika mzozo wanaamua wanachojadilia na wanachokubaliana.

Wapatanishi ni wadilifu na hawaegemei upande wowote au kutoa ushauri wa kisheria.

Zaidi ya asilimia 85 ya mapatanisho yanamalizika kwa kufikia mwafaka. Mara nyingi mapatanisho yanaweza kupangwa haraka na kuchukua masaa 2-4.

#### **Mizozo ipi inaofaa kwa upatanisho?**

CJC inaweza kukusaidia kwenye aina nyingi ya mizozo ikiwemo:

- Mizozo ya jumua ya mitaa / ya ujirani kuhusu vitu kama vile ua, kelele, wanyama kipenzi, miti, uharibifu wa rasilimali na tabia za watu
- Mawasiliano mahali pa kufanyia kazi
- Vyama au mashirika ambayo wanachama wako kwenye mzozo
- Mawasiliano kati ya wanafamilia
- Madai madogo / madai yenye kuhusu raia
- Mikutano na walioathiriwa na uvunjaji wa sheria
- Aina nyingine za mzozo

#### **Namna ya kupanga upatanisho**

Unaweza kukipa simu kwenye namba ya bure, kuandika, kutuma barua pepe au kutuzuru wewe mwenyewe.

Huduma bure ya mkalimani inapatikana.

Wakati unaita CJC wafanyakazi wetu wenye uzoefu wata:

- Zungumza na wewe kuhusu tatizo na kujadiliana njia unaweza kusuluhisha

tatizo lako wewe mwenyewe

- Toa taarifa na / au udhamini
- Kadiria kwamba mzozo wako unafaa kwa upatanisho na kama ni vile, kuomba taarifa fupi kuhusu wewe, matatizo yako na watu wengine wanaohusika ; na
- Kwa idhini yako, tutawasiliana na watu wengine ili kupanga upatanisho kwa muda unaofaa kwa nyie wote wawili.

Mapatanisho yanaweza kupangwa wakati wa kutwa, jioni au mwishoni mwa wiki.

Mapatanisho yanafanyika kwenye Kituo cha Haki za Jumua Darwin au mahali panapofaa mitaani katika Eneo nzima.

Mikutano kwa njia ya simu inaweza kupangwa pia.

### **Mawasiliano**

Kwa taarifa zaidi na msaada:

Simu: 1800 000 473

Faksi: 08 8981 3812

Barua pepe: [cjc.doj@nt.gov.au](mailto:cjc.doj@nt.gov.au)

Tuma barua:

GPO BOX 1722

DARWIN NT 0801

Zuru wewe mwenyewe kwenye:

Gorofa la 7

Level 1 Darwin Magistrates Court

Nichols Place

Darwin NT 0800